

TOLEO LA 4

Salamu kwa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Wakati unakwenda kwa haraka. Tunakaribia kufungua shule tena. Nimepata kufahamu mengi kuhusu wilaya kwa kufanya mikutano ya ana kwa ana na wafanyakazi, viongozi wa wazazi na familia, na kuzoea kaunti hii nzuri ambayo sasa ninaiita nyumbani.

Nimekuwa na wiki yenye shughuli nyingi nikisafiri kote katika Kaunti ya DeKalb, na nimependezwa na tofauti ulioko wa watu. Shukrani kwa Msimamizi wa Elimu wa Eneo Trenton Arnold kwa kuwa mwenyeji mzuri na kusafiri pamoja nami katika Eneo la II. Wiki hii, nilitembelea Shule ya Upili ya Druid Hills, Shule ya Msingi ya Fernbank, Shule ya Msingi ya Smoke Rise, Shule ya Msingi ya Idlewood na Shule ya Msingi ya Midvale. Pia nilipata nafasi ya kutembelea Kituo cha Kimataifa cha Wageni na Kituo cha Family Impact, ambavyo huhudumia familia na wanafunzi zetu.

Wakati wa ziara zangu za Siku ya Jumatano ya Kutembelea Eneo Kazi, kile nilichojuua kilipata kuthibitishwa; kwamba Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb ni ya kipekee sana. Kila shule ina sifa, utamaduni, mtindo na uwepo wake wa kipekee. Natazamia siku ambayo nitaweza kukutana na wanafunzi, familia na wafanyakazi wetu zaidi.

Tunapokaribia siku kuu, tarehe 17 Agosti, kumbuka kuwa ingawa maisha ni tofauti, elimu bado ni daraja ya fursa katika ulimwengu. Bado tuna fursa ya kujifunza, kufikia, kuwa na ndoto, kukua na kupanga mipango. Natumai kwamba utasherehekea Siku ya Kurudi Shuleni 2020 kwa njia ya mtandaoni, na utajiandaa kwa mwaka wa kufurahisha kwa sababu Pamoja Tunaweza Kuamini na Kufanikisha, hata kama hali sio ya kawaida. Ninabaki kuwa na shauku kuhusu masomo ya mtandaoni. Najua walimu wetu wanaunda fursa zitakazowashirikisha wanafunzi wao.

Ningependa kutoa shukrani maalum kwa mfanyakazi ambaye aliwahi kuwa afisa mkuu wa muda wa rasilimali watu—mara mbili—na kuongoza wilaya hii kwa ujasiri na furaha. Sijamfahamu kwa muda mrefu, lakini najua tutamkosa sana. Bi. Linda Woodard, shukran kwa huduma zako. Tunakutakia kila la kheri katika shughuli zako za siku zijazo.

Mwishowe, familia ya DeKalb, natumai kwamba utajiunga nasi kwenye mitandao ya kijamii (Facebook, Twitter na Instagram) tarehe 10-13 Agosti, tunapojiandaa kwa mwaka mpya wa shule. Jitayarisha kupiga picha za kufurahisha na kushiriki kumbukumbu na vidokezo vya kuisimua.

Shukran tena kwa maoni yako yote katika wiki tatu zilizopita. Angalia maelezo maalum kutoka kwa Kituo cha Family Impact.

Shabiki wenu #1,

Cheryl Watson-Harris, Msimamizi